# Vielezi vya Mahali katika Kiswahili na Kimashami

*B. P. Lema*

*Ikisiri*

Lugha zote duniani zimewekwa katika makundi kwa kuzingatia vigezo mbalimbali kama vile kushabihiana katika vipengele fulani vya kiisimu. Ni kwa mantiki hiyohiyo lugha za Kibantu zimewekwa katika kundi moja. Hata hivyo ,lugha zilizomo kwenye kundi moja bado hufanana katika vipengele fulani na kutofautiana katika vipengele vingine. Lugha za Kibantu, pamoja na kufanana sana, hutofautiana katika vipengele mbalimbali. Katika makala haya Kiswahili na Kimashami, ambazo ni lugha za Kibantu, zimetumika kuonesha tofauti iliyopo katika kueleza mahali kitu kilipo. Kimsingi inaonekana kuwa Kiswahili kina mbinu mbili zinazotumika kuonesha kitu kilipo. Mbinu ya kwanza ni kutumia kiambishi tamati {–ni} kwenye nomino inayowakilisha mahali. Mbinu ya pili ni matumizi ya mofimu huru {kwenye}. Hata hivyo, mbinu hizi mbili hazitumiki kwa uhuru kwani matumizi yake yamewekewa mipaka ya kipragmatiki. Lakini pia mbinu hizi mbili haziwezi kutumika kwa wakati mmoja kwani matumizi ya mbinu ya kwanza huzuia matumizi ya mbinu ya pili. Hali hii ni tofauti sana katika lugha ya Kimashami. Kwanza Kimashami hutumia mbinu nyingi zaidi ikilinganishwa na Kiswahili. Kwa mfano, pamoja na kutumia kiambishi tamati {–ni} kama ilivyo kwa Kiswahili, Kimashami hutumia pia kiambishi tamati {–u}, kiambishi tamati kapa- {*ø*} na mofimu huru {ifo}. Matumizi ya viambishi tamati katika Kimashami hayatofautiani sana na yale ya lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu si kila kiambishi tamati cha mahali kinaweza kutumiwa kwa kila neno. Hata hivyo, katika Kimashami ni kawaida kutumia viambishi tamati na mofimu huru kwa pamoja bila athari yoyoye ya kisemantiki, kipragmatiki au kisintaksia.

## 1.0 Utangulizi

Lugha zote duniani zina namna mbalimbali ya kueleza kulingana na mahitaji ya mawasiliano kwa watumiaji wake. Taarifa hizo ni pamoja na nyakati, minyambuliko ya vitenzi na mahali. Lugha hutumia maumbo mbalimbali ya maneno ili kuwasilisha taarifa inayohusika. Makala haya yamelenga kuonesha jinsi ambavyo Kiswahili na Kimashami hutofautiana katika kuonesha mahali vitu vilipo, kwa kutumia viambishi na mofimu huru. Makala yameanza na usuli wa lugha lengwa, yaani Kiswahili na Kimashami, ikifuatiwa na mjadala wa vielezi vya mahali na hatimaye kuhitimisha mjadala kwa kutoa majumuisho.

## 2.0 Usuli wa Lugha Lengwa

Kiswahili ni moja kati ya lugha zilizosambaa sana Afrika. Kulingana na mtaalamu Guthrie (1967-1971), Kiswahili kimepewa namba ya utambulisho ya G42, kwa maana kuwa lugha hii iko katika kanda G kundi la 40, na ni lugha ya pili katika kundi hilo. Kiswahili ni lugha inayotumika sana katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, na hasa katika nchi za Tanzania, Kenya, Uganda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (Chiraghdin na Mnyampala, 1977; Heine, 1990; Khamisi, 1974; Mbaabu, 1991). Kiswahili ni lugha ya taifa la Tanzania, na lugha ya kufundishia katika ngazi ya shule za msingi (Mulokozi,

2007; Whiteley, 1969). Kwa mujibu wa Rugemalira na Muzale (2009), Kiswahili kina wazungumzaji asilia wapatao 2,379,294. Kimashami, kwa upande mwingine, ni moja kati ya lugha ndogondogo nyingi nchini Tanzania zinazozungumzwa katika maeneo machache ya nchi. Namba ya utambulisho wa Kimashami kwa mujibu wa Guthrie ni E62, kwa maana kwamba iko katika kanda E kundi la 60, ambapo ni lugha ya pili katika kundi hilo. Kimashami kinazungumzwa katika wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro. Lugha hii hutumika zaidi katika mazungumzo ya kila siku yasiyo rasmi, uzalishaji na hata katika uendeshaji wa ibada za kikristo (Kilutheri). Kwa mujibu wa Rugemalira na Muzale (2009), Kimashami kina wazungumzaji asilia wapatao 194,868.

## 2.1 Mifumo ya sauti

Kufuatana na maandiko yaliyopo katika Kiswahili na Kimashami, kuna ushahidi kwamba lugha hizi hazina tofauti yoyote katika irabu kwani zina irabu zipatazo tano kila moja, huku irabu zote zikiwa fupi. Vilevile, irabu hizo hutamkwa kwa namna inayofanana katika lugha hizi mbili. Hata hivyo, tofauti katika matamshi ya irabu kwenye lugha hizi hutokana na ukweli kuwa Kimashami ni lugha yenye toni. Kwa upande wa konsonanti, lugha hizi pia hufanana kwa kiasi kikubwa kwani konsonanti zinazotokea kwenye Kiswahili hupatikana pia katika Kimashami. Hata hivyo, tofauti kubwa ipo katika sifa bainifu za sauti hizo kwa kigezo cha guna. Konsonanti za Kiswahili zinaweza kuwa na sifa ya *guna* na *si-guna*. Kwa upande wa Kimashami, ushahidi unaonesha kuwa, isipokuwa tu kwa ***/t/*** na ***/d/***, pale konsonanti inapokuwa na sifa ya *guna*, au kinyume chake, basi konsonanti ya upande wa pili huwa haipo kabisa katika lugha hiyo. (Yukawa, 1989; Phillipson, 2003; Rugemalira na Phanuel, 2012). Kwa mfano, konsonanti zifuatazo zina sifa ya *si-guna*:

1. a. /**s**/ - **s**ubha (*kondoo dume)*
   b. /**ʃ**/- ***sh***onga (*chakula)*
   c. /**k**/- ***k***ikwa *(kiazi kikuu)*
   d. /**f**/- ***f***unga *(vumbi)*

Hivyo, konsonanti ni hizohizo lakini zenye sifa ya guna (/**z**/, /**g**/ na /**v**/) hazimo katika orodha ya konsonanti za Kimashami. Halikadhalika, konsonanti zifuatazo zina sifa ya guna, na hivyo zile za upande wa pili zenye sifa ya si-guna hazipatikani katika Kimashami.

2. a. /**b**/ - ***b***iri (*kisogo)*
   b. /**gh**/- mu***gh***a (*maji)*

Hata hiyo, katika vipengele vingine, hasa konsonanti kutanguliwa na ving'ong'o, hakuna ushahidi, kwamba lugha hizi hutofautiana, kama inavyojidhihirisha katika data ifuatayo:

| | | Kiswahili | Kimashami | |
|---|---|---|---|---|
| 3. | a. | ***mb***aazi | ***mb***ughu | *(mbuzi)* |
| | b. | a***nd***azi | ***nd***afu | *(beberu aliyehasiwa)* |
| | c. | ***nz***i | ***ns***ighi | *(mkaa)* |

Katika mifano hii ni dhahiri kwamba lugha hizi zote zina sifa ya konsonanti fulani za lugha kutanguliwa na konsonanti katika muundo wa maneno.

## 3.0 Vielezi vya Mahali

Kama ilivyokwishabainishwa hapo juu, Kiswahili na Kimashami ni lugha zinazofanana hasa ikizingatiwa kwamba zote ni lugha za Kibantu. Pamoja na kufanana katika vipengele vichache vilivyobainishwa (taz. § 2.1), lugha hizi pia hufanana katika vielezi mbalimbali na hasa vile vya mahali, ambavyo ndivyo kiini cha mjadala huu. Kipengele cha kwanza katika kufanana kwa vielezi katika lugha hizi ni ukweli kwamba lugha hizi hutumia kiambishi tamati {–ni} kama inavyodhihirishwa katika data ifuatayo:

| | | *Kiswahili* | *Kimashami* |
|---|---|---|---|
| 4. | a. | chura yuko maji***ni*** | kilwa kikee mughe***n*** |
| | b. | binti yule amebeba chungu kichwa***ni*** | mfu ulya abhikye nungu ngho***n*** |
| | c. | weka hicho kitabu meza***ni*** | bhika kitabu ikyo mesa***n*** |

Katika data hiyo inaonekana kwamba lugha hizi mbili hufanana katika matumizi ya kiambishi tamati {*-ni* } kuonesha mahali kilipo kitu. Hata hivyo, katika data ya Kimashami, kiambishi tamati {***-ni***} kinaathiriwa na mchakato wa kimofofonolojia ujulikanao kama *udondoshaji wa irabu*. Kwa mujibu wa data hii ni kwamba irabu /i/ ya Kimashami hudondoshwa pale ambapo inatanguliwa na king'ong'o /n/ mwishoni mwa neno. Katika Kiswahili kanuni hii huonekana sana kwenye nomino zinazoishia na silabi – **$mu$** ambapo irabu /u/ hudondoka na hivyo kupata **m**aneno kama mwali***m***, maalu***m***, mtaalamu na mengine, hasa katika matamshi.

Hata hivyo, data hii inaweza kutoa taswira ya jumla kwamba lugha hizi mbili hufanana katika maneno yanayoweza kupokea kiambishi tamati ***–ni*** cha mahali, ilhali hali ya mambo haiko hivyo hata kidogo. Kwa mfano, katika Kiswahili si sahihi kutumia nomino kama vile unga, chai, chakula, simu, uji na nyinginezo kwa kufuata utaratibu unaoonekana kwenye data ya (4) a-c hapo juu. Data ifuatayo inaonesha hali halisi kuhusiana na ruwaza hii.

5. a. *ili kupata uji, tia maji unga***ni***
   b. *leta sukari tutie chai***ni***
   c. *weka chumvi zaidi chakula***ni***
   d. *simu***ni*** kuna muda wa maongezi?

Data hii inaweza kuwa sahihi endapo neno ***kwenye*** litachopekwa kabla ya nomino inayohusika. Mchakato huu hufunga milango ya matumizi ya kiambishi tamati {–ni} kama inavyoonekana katika data ifuatayo:

6. a. ili kupata uji, tia maji ***kwenye*** unga
   b. lete sukari tutie ***kwenye*** chai
   c. weka chumvi zaidi ***kwenye*** chakula
   c. k***wenye*** simu kuna muda wa maongezi?

Kwa kurejea data ya 5a-c na 6a-c ni dhahiri kwamba Kiswahili huchagua nomino za mahali ambazo zinaweza kutumiwa pamoja na kiambishi tamati {–ni}. Hili ni suala linalohitaji utafiti makini zaidi ya makala haya ili kubaini vigezo vya utenzi huo. Suala la pili ni kwamba pale ambapo si sahihi kutumia kiambishi tamati {–ni} katika Kiswahili mbinu nyingine hutumika, yaani kutumia neno ***kwenye***. Matumizi ya neno ***kwenye***, huondoa kabisa uwezekano wa kutumia kiambishi tamati {–ni}. Hivyo mbinu hizi mbili hutumiwa moja moja kama mbadala wa nyingine. Kwa lugha ya kitaalamu, mbinu hizi hutumiwa katika *mgawanyo wa kimtoano* ( Massamba, 2004). Hii ina maana kwamba, pale ambapo {–ni} inatumika, {kwenye} haitumiki kabisa.

Kwa upande mwingine Kimashami kinatofautiana na Kiswahili katika kuchagua maneno ambayo yanaweza kutumiwa herufi pamoja na kiambishi tamati {-ni}. Kwa mfano, katika data inayoonekana katika (5), matumizi ya kiambishi tamati {-ni} yanayogoma katika Kiswahili yanakubalika bila tatizo katika Kimashami kama inavyoonekana katika data ifuatayo:

| | **Kimashami** | **Kiswahili** |
|---|---|---|
| 7. a. | bhika mugha nswe***n*** | 'tia maji ***kwenye*** unga' |
| b. | ende sukari lubhike shai***n*** | 'lete sukari tutie ***kwenye*** chai' |
| c. | bhika shumbi ingi shonge***n*** | 'weka chumvi zaidi ***kwenye*** chakula' |
| c. | tiifo ileghi simu***n?*** | '***kwenye*** simu kuna muda wa maongezi (pesa)?' |

Katika data hii ni dhahiri kwamba Kimashami na Kiswahili zinatofautiana sana katika uchaguzi wa maneno ambayo yanaweza kutumiwa pamoja na kiambishi tamati {-ni}. Hii ni changamoto kubwa kwa mmilisi wa Kimashami anayetaka kujifunza Kiswahili. Kuna uwezekano mkubwa wa mmilisi wa Kimashani kufanya makosa ya kisarufi katika Kiswaili kutokana na athari za lugha mama. Kwa misingi hiyo, ni wajibu wa walimu wa Kiswahili katika maeneo

mbalimbali nchini kuzingatia uzoefu wa wanafunzi na athari ya lugha zao za awali.

Tofauti nyingine kubwa kati ya Kiswahili na Kimashami ni matumizi ya mbinu zote mbili, yaani kiambishi tamati {–ni} na mofimu huru {kwenye}, ni kwamba katika Kimashami mbinu hizo zinaweza kutumika kwa wakati mmoja, wakati katika Kiswahili matumizi ya mbinu mbili kwa kwa pamoja hayawezekani. Katika data ifuatayo ya Kimashami, mofimu huru {kwenye} katika Kiswahili inawakilishwa na mofimu huru {ifo}. {Ifo} na {-ni} katika Kimashani zinaweza kutokea pamoja katika muktadha wa tungo.

| | **Kimashami** | **Kiswahili** |
|---|---|---|
| 8. a. | bhika mugha ***ifo*** nswe***n*** | 'tia maji ***kwenye*** unga' |
| b. | ende sukari lubhike ***ifo*** shai***n*** | 'lete sukari tutie ***kwenye*** chai' |
| c. | bhika shumbi ingi ***ifo*** shonge***n*** | ' 'weka chumvi zaidi ***kwenye*** chakula' |
| c. | iifo ileghi ***ifo*** simu***n***? | '***kwenye*** simu kuna muda wa maongezi?' |

Katika data hii inaonekana kwamba katika Kimashami matumizi ya mbinu zote mbili kuelezea mahali yanaruhusiwa bila kuathiri mchakato wowote wa kisintaksia ikilinganishwa na Kiswahili. Kwa mfano, katika Kiswahili mofimu huru {kwenye} hutumika kabla ya neno husika, sawa na Kimashami hata kama mbinu zote zitatumiwa pamoja.

Swali la msingi hapa ni kuwa: Je, kuna kanuni au ruwaza gani katika uhuru huu? Hili ni swali la msingi kwa sababu kulingana na mjadala wa data za Kimashami, ni rahisi kudhani kwamba kwa vile tunaweza kutumia kiambishi tamati {-ni} bila kulazimika kutumia mofimu huru {ifo}, basi tunaweza pia kutumia mofimu huru {ifo} bila kulazimika kutumia kiambishi tamati {–ni}. Hata hivyo, utaratibu huu si sahihi kabisa. Hii ni kusema kwamba data ifuatayo haikubaliki katika Kimashami.

| | **Kimashami** | **Kiswahili** |
|---|---|---|
| 9. a. | *bhika mugha ***ifo*** nswa | 'tia maji *kwenye* unga' |
| b. | *ende sukari lubhike '***ifo*** shai | 'lete sukari tutie *kwenye* chai' |
| c. | *bhika shumbi ingi ***ifo*** shonga | 'Weka chumvi zaidi *kwenye* chakula' |
| c. | * ***ifo*** simu tiifo pesa? | '*kwenye* simu kuna muda wa maongezi?' |

Kwa mujibu wa data hii, ni sahihi kabisa kudai kwamba {ifo} siyo kielezi cha mahali bali ni kiashiria cha uwepo wa kiambishi cha mahali. Hivyo, {ifo} huashiria kuwepo kwa kiambishi tamati {-ni} kwenye nomino inayofuatia kama ilivyodokezwa hapo awali. Hii ni kwa sababu {ifo} haiwezi kutokea peke yake bila kuwepo kiambishi tamati cha mahali.

Awali imeonekana kwamba siyo kila nomino ya katika Kiswahili inaweza kuchopekwa kiambishi tamati {–ni} na kwamba kiambishi {–ni} na mofimu neno huru {kwenye} hutokea katika mgawanyo wa kimtoano, kwa maana kwamba pale ambapo {-ni} inatokea, basi {kwenye} haiwezi kutokea. Huu ndio msingi wa kujenga hoja dhidi ya neno huria {ifo} katika Kimashami kama kielezi cha mahali. Badala yake kimeitwa kiashiria cha uwepo wa kielezi cha mahali kama kinavyowakilishwa na moja kati ya vielezi vya mahali katika Kimashami. Ushahidi zaidi kuhusu suala hili unadhihirishwa katika mjadala kuhusu vielezi vingine katika Kimashami katika aya zinazofuata.

Kama ilivyodokezwa hapo awali, (taz. ikisiri) viambishi tamati vingine vya mahali katika Kimashami ni {-u} na (Ø). Uchaguzi katika nomino za mahali ambazo zinaweza kutokea pamoja na viambishi hivi uko dhahiri zaidi ikilinganishwa na {–ni}. Kwanza kabisa, idadi ya nomino za mahali zinazotumika pamoja na viambishi hivyo ni ndogo sana. Kwa kuanza na kiambishi tamati {-u} inaonekana kwamba kiambishi hiki kinaweza kutumika kuonesha kwamba kuna hali fulani ya mwinuko mahali panapoelezwa. Kwa mfano, kiambishi hiki hutumika pamoja na maneno kama *paa, mlima*, *mawingu* na *mbingu* kama inavyoonekana katika data ifuatayo:

| | | Kimashami | Kiswahili |
|---|---|---|---|
| 10. | a. | ndeye ikee mmbe*u* | 'ndege yuko juu ya paa |
| | b. | kuyo nndu alya ifumbu*u* | 'kuna mtu kileleni mwa mlima |
| | c. | irubha akee irubhe*u* | 'Mungu yuko mbinguni |
| | d. | matuu akee ngine*u* | 'mawingu yapo angani' |

Kama data hiyo inavyoonesha, kiambishi {-u} hubeba dhana ya kitu kuwa juu ya mahali. Hivyo basi kiambishi hiki hutumia zaidi kigezo cha semantiki katika uchaguzi wa nomino zinazowakilisha mahali.

Mbinu nyingine katika Kimashami ya kuonesha kilipo kitu ni matumizi ya kiambishi tamati kapa {Ø}. Hata hivyo, mbinu hii hutumika katika idadi ndogo sana ya nomino. Mifano ifuatayo inaweza kuwa ndio maneno pekee ambayo mofimu tamati kapa inaweza kujitokeza:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 10. | a. | maru akee kaiØ | 'ndizi ziko darini' |
| | b. | ata ngashe mmbaØ | 'mpeleke ndama ndani (ya nyumba)' |
| | c. | bhika mwana mungoØ | 'mbebe mtoto mgongoni' |

Kulingana na data iliyotangualia hapo juu, inaweza kudaiwa kwamba matumizi ya kiambishi tamati kapa pia, kwa kiasi fulani, hutumia kigezo cha semantiki katika kuchagua nomino ambazo zinaweza kupachikwa kiambishi hiki.

Kimsingi, kiambishi tamati kapa pia huweza kutumika pamoja na mofimu huria {ifo} kama ilivyo kwa vielezi vingine vya mahali.

## 4.0 Hitimisho

Katika makala haya tofauti ya vielezi vya mahali katika Kiswahili na Kimashami imeainishwa kwa kuzingatia maumbo mbalimbali kama yanavyojidhihirisha katika nomino zinazoonesha mahali. Jambo la msingi kabisa ni kwamba Kiswahili na Kimashami hutumia zaidi kiambishi tamati {-ni}. Hata hivyo, Kiswahili kinaonekana *kuminya sana* nomino za mahali zinazoweza kutumiwa pamoja na {–ni} ikilinganishwa na Kimashami. Pia, imeonekana bayana kwamba Kiswahili kina njia mbili tu za kuelezea kitu kilipo. Mbinu hizo ni matumizi ya kiambishi tamati {–ni} na neno huru {*kwenye*} ambapo mbinu hizi hutumika pamoja na kwa wakati mmoja. Hali hii ambayo tumeiita *mgawanyo wa kimtoano* inaonekana pia katika lugha ya Kimashami ambapo tumeona takriban mbinu tatu zikitumika, yaani viambishi tamati {–ni}, {-u} na kapa {*-ø*}. Tabia hii ya kimtoano inaweza kuwa changamoto kwani inaweza kudaiwa kwamba ndiyo tabia ya lugha zote za Kibantu. Hata hivyo, ni vigumu kuhitimisha hivyo hadi tupate data kutoka katika lugha mbalimbali, na hasa zile za Kibantu. Katika mjadala wa hoja mbalimbali zilizochomoza katika makala haya, changamoto iliyo dhahiri lakini pia muhimu kushughulikiwa, ni kuweza kugundua vigezo vinavyozingatiwa katika kuchagua nomino zinazoweza kutumiwa pamoja na kielezi fulani. Hili ni eneo muhimu sana ambalo wanaisimu wanaweza kuliangalia kwa undani zaidi.

## MAREJEO

Chiraghdin, S. na M. Mnyampala. (1977). *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: O.U.P.

Guthrie, M. (1967-71). *Comparative Bantu: An Introduction to the Comparative Linguistics and Prehistory of the Bantu Languages*. Juz. 4 Farnborough: Gregg Press.

Heine, B. (1990). Kiswahili [from *Sprache, Gesselschsft und Communikation*], katika Legère, K. (Mhariri), uk. 25-48.

Khamisi, A.M. (1974). Swahili as a National Language. Katika *Towards Ujamaa* uk. 288-308. na G. Ruhumbika (mhariri), Kampala, Nairobi na Dar es Salaam: EAPH.

Legere, K. (1990). Recent Development of Kiswahili. Katika Léger, K. (mhariri): 49-84.

Massamba, D.P. B. ( 2004). *Kamusi ya Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Mbaabu, I. (1991). *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili*. Nairobi: Longman.

Mulokozi, M. M. (2007). Kiswahili as a National and International Language.www.helsinki.fi/hum/aakl/documents/kiswahili.pdf iliyosomwa tarehe 18 Januari, 2011.

Rugemalira, J. na H.R.T. Muzale (2009). *Atlasi ya Lugha za Tanzania*. Dar es Salaam: LOT Publications.

Rugemalira, J. na B. Phanuel, (2012). A Grammatical Sketch of Mashami. *Occasional Paper in Linguistics*. Dar es Salaam: LOT Publications.

Whiteley, W. (1969). *Swahili: The Rise of a National Language*. London: Methuen.